JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

## URAIA NA MAADILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI ....... 2

2.1 Sehemu A ........................................................................................ 2

2.1.1 Kuchagua herufi ya jibu sahihi ........................................................................................ 2

2.1.2 Kuoanisha maana ya maneno ........................................................................................ 8

2.1.3 Kuchagua jibu sahihi katika mabano ........................................................................................ 12

2.2 Sehemu B ........................................................................................ 17

2.2.1 Kuoanisha matendo ........................................................................................ 17

2.2.2 Kuchunguza picha ........................................................................................ 21

2.2.3 Kusoma kifungu cha habari ........................................................................................ 26

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........................................................................................ 30

4.0 HITIMISHO ........................................................................................ 31

5.0 MAPENDEKEZO ........................................................................................ 31

Kiambatanisho A ........................................................................................ 33

Kiambatisho B ........................................................................................ 34

## DIBAJI

Baraza la Mitihani limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2020. Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera na wadau wengine wa elimu kuhusu maarifa, stadi na ujuzi ambao wanafunzi waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka miwili ya Elimu ya Msingi. Hivyo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu, unaweza kutumika kama kipimo cha ufanisi katika utekelezaji wa mtaala huo kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu inayowajengea wanafunzi uwezo katika umahiri mbalimbali wa somo la Uraia na Maadili.

Katika taarifa hii, dosari na mambo mbalimbali ambayo yamechangia wanafunzi kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi yameainishwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa umahiri mbalimbali, na kushindwa kuhawilisha maarifa. Aidha, chati ya ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kwa mwaka 2019 na 2020 imewekwa mwishoni mwa taarifa hii kuonesha jinsi wanafunzi walivyofaulu katika kila umahiri uliopimwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa ya wanafunzi.

Mwisho, Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe 26 mwezi November mwaka 2020. Jumla ya wanafunzi 1,828,265 waliandikishwa kufanya upimaji ambapo wanafunzi 1,702,775 sawa na asilimia 93.1 walifanya upimaji huu. Aidha, ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,702,775 sawa na asilimia 95.46 walifaulu, na wanafunzi 77,370 sawa na asilimia 4.54 hawakufaulu. Ufaulu huu umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo wanafunzi 1,584,685 (95.26%) walifaulu na wanafunzi 78,853 (4.74%) hawakufaulu.

Upimaji ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yenye jumla ya vipengele 25, yaliyogawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 13 vyenye jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 12 vyenye jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote A na B. Upimaji ulikuwa na ujumla ya alama 50.

Katika sehemu A, wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku, kuoanisha maana ya maneno katika fungu A na maneno husika katika fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi, na kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Aidha, katika sehemu B, wanafunzi walitakiwa kuweka alama ya vema kwenye sehemu inayohusika, kuchunguza picha kisha kujibu maswali na kusoma kwa umakini kifungu cha habari na kujaza sehemu zilizoachwa wazi.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa somo la Uraia na Maadili itajikita katika kuangalia maswali yote sita yaliyotoka katika umahiri mbalimbali ulioainishwa katika muhtasari. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi ya asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuchagua jibu sahihi na sababu zilizofanya wachague majibu hayo.

Viwango vya kufaulu kwa kila swali vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Iwapo asilimia 0 – 33 ya wanafunzi waliweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango cha ufaulu cha swali hilo ihesabika kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 – 66, ufaulu kwa swali hilo ulihesabika kuwa ni kwa wastani na kiwango cha ufaulu kinahesabika kuwa ni kizuri iwapo watahiniwa walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 – 100. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa wanafunzi ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu kwa kiwango cha wastani na ufaulu hafifu unawakilishwa na rangi nyekundu.


# 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

## 2.1 Sehemu A

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi na lilikuwa na vipengele vitano ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2 vilikuwa na jumla ya alama 10. Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha maana ya maneno katika fungu A na maneno husika katika fungu B kwa kuandika jibu sahihi katika karatasi ya kujibia na ilikuwa na vipengele vinne kila kipengele kilikuwa na alama 2 jumla ya alama 8. Swali la 3 lilikuwa la kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika karatasi ya kujibia na lilikuwa na vipengele vinne, kila kipengele kilikuwa na alama 2 jumla ya alama 8. Jumla ya alama katika sehemu hii ni 26.

### 2.1.1 Kuchagua herufi ya jibu sahihi

Swali **la 1** ndilo lililojibiwa vizuri zaidi ikilinganishwa na maswali mengine. Swali liliwataka wanafunzi kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku. Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kudumisha amani*. Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, wanafunzi 1, 252,142 sawa na asilimia 73.6 walifaulu. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 1.1.




**Chati Na. 1:** Kiwango kizuri cha ufaulu cha wanafunzi katika swali la 1 kwa kupata kati ya alama 4 hadi 10.

Chati Na.1: inaonesha kuwa wanafunzi wengi katika swali la 1 walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ambapo asilimia 73.6 ya wanafunzi walipata alama kuanzia 4 hadi 10.

Wanafunzi waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha katika umahiri wa *Kudumisha amani* ikilinganishwa na umahiri mwingine uliopimwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Ngoma ya asili ya watu wa mkoa wa Ruvuma huitwa
- A mganda
- B mdundiko
- C mdumange
- D sindimba

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti* na kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutambua ngoma mbalimbali za asili zinazochezwa maeneo mbalimbali ya Tanzania. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi, *A*, *Mganda* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya aina mbalimbali za ngoma za asili za Tanzania na hivyo waliweza kutambua kwamba ngoma ya Mganda ni ngoma ya asili ya watu wa mkoa wa Ruvuma.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *B*, *Mdundiko, C*, *Mdumange* na *D*, *Sindimba* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya aina mbalimbali za ngoma za asili za Tanzania kwa kila kabila. Kwa mfano wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Mdundiko* hawakujua kuwa mdundiko ni ngoma ya asili ya watu wa mikoa ya Pwani na Dar es salaam. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C*, *Mdumange* hawakujua kuwa mdumange ni ngoma ya asili ya watu wa mkoa wa Tanga. Aidha, kipotoshi *D*, *Sindimba* kiliwavutia wanafunzi ambao hawakujua kuwa sindimba ni ngoma maarufu ya asili ya watu wa mkoa wa Mtwara.

(ii) Moja kati ya mambo yanayovutia watalii katika nchi ya Tanzania ni
- A barabara na ufugaji wa kuku
- B bustani za maua na mvua
- C milima na hifadhi za taifa
- D viwanja vya michezo na mabwawa ya samaki

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kujenga urafiki mwema na mataifa mengine* na kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutambua vivutio mbalimbali vya utalii vinavyopatikana Tanzania. Wanafunzi waliobaini jibu sahihi C, *Milima na hifadhi za taifa* walikuwa na uelewa juu ya maana ya vivutio na aina za vivutio vya utalii vinavyopatikana nchini Tanzania. Tanzania imekuwa ikipokea watalii wengi kutoka mataifa mbalimbali kutokana na kuwa na vivutio mbalimbali kama vile mlima Kilimanjaro, hifadhi mbalimbali za wanyamapori kama Serengeti, Ngorongoro, Mikumi, Selous na kisiwa kama vile Zanzibar chenye historia ya kuwahi kuwa kituo cha biashara ya utumwa karne zilizopita. Aidha, vivutio kama vile hifadhi za wanyamapori zina wanyama wa aina mbalimbali wanaopatikana kwa wingi Tanzania pekee kama vile Tembo, Simba, Twiga, Nyumbu, Nyati, Chui, Duma n.k.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *A*, *Barabara na ufugaji wa kuku, B*, *Bustani za maua na mvua,* na *D*, *Viwanja vya michezo na mabwawa ya samaki* hawakuwa na uelewa juu ya vitu mbalimbali vinavyovutia watalii nchini. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A*, *Barabara na ufugaji wa kuk*u walishindwa kubaini kuwa lengo kuu la kuwa na barabara ni kurahisisha usafirishaji wa

watu na bidhaa mbalimbali. Aidha, ufugaji wa kuku una lengo la kuwapatia wananchi kitoweo au biashara inayoweza kuwapatia wananchi mapato yanayoweza kusaidia kukidhi mahitaji ya kikundi au mtu binafsi. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B*, *Bustani za Maua na mvua* walishindwa kuelewa kuwa maua ni zao la biashara au kupamba maeneo ya nyumbani na sehemu nyingine za umma hususani mijini. Aidha, uwepo wa mvua husaidia sana shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na bustani za maua. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *Viwanja vya michezo na mabwawa ya samaki,* walishindwa kubaini kuwa viwanja vya michezo hutumika kwa michezo mbalimbali yenye lengo la kutoa burudani kwa wananchi, kuingiza kipato na kuongeza utimamu wa mwili kwa wanaoshiriki katika michezo. Michezo hiyo ni ya aina mbalimbali na huhusisha mashindano ya ndani ya nchi na michezo ya kimataifa. Mfano mchezo wa mpira wa miguu unapendwa na watu wengi Tanzania lakini siyo kivutio cha utalii. vilevile, lengo la kujenga mabwawa ya samaki ni kupata kipato na kitoweo kutokana na ufugaji wa samaki. Pia ufugaji wa samaki husaidia kupunguza tatizo la uvuvi haramu kwa kuongeza upatikanaji wa samaki kwa njia halali.

(iii) Zipi kati ya nchi zifuatazo **sio** wanachama wa jumuiya ya Afrika mashariki?

A Tanzania na Uganda
B Kenya na Uganda
C Rwanda na Burundi
D Zambia na Zimbabwe

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *Kujenga Urafiki Mwema na Mataifa Mengine* na kililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kufahamu nchi ambazo sio wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki. Wanafunzi walioandika jibu sahihi *D*, *Zambia na Zimbabwe*, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya nchi sita wanachama zinazounda jumuiya ya Afrika Mashariki sita ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani ya Kusini. Wanafunzi hao walipaswa kujua kuwa Zambia na Zimbabwe ni wanachama wa Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *A*, *Tanzania na Uganda*, *B*, *Kenya na Uganda* na *C*, *Rwanda na Burundi*, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya nchi ambazo sio wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi zote zilizotajwa katika vipotoshi vya *A*, *Tanzania na Uganda*, *B*, *Kenya na Uganda* na *C*, *Rwanda na Burundi* ni wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) Shughuli gani ya asili inayofanywa na jamii ya watu waishio karibu na bahari au maziwa?

A Ufugaji wa samaki.
B Uchimbaji mabwawa
C Uvuvi wa samaki
D Kilimo cha mpunga.

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kuchangamana na watu wenye asili tofauti* na kililenga kubaini shughuli zinazofanywa na watu wanaotoka kanda au sehemu tofauti nchini, ikihusisha shughuli kama vile ufugaji wa ng'ombe, kilimo na uvuvi ambazo huamuliwa na jiografia ya eneo husika.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *C, uvuvi wa samaki*, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya shughuli mbalimbali za asili zinazofanywa na watu wanaoishi karibu na bahari na maziwa. Wanafunzi hawa walitambua kuwa watu wengi waishio karibu na maji makuu kama vile bahari na maziwa shughuli yao kubwa ni uvuvi wa samaki. Aidha, Jamii nyingi zinazokaa karibu na maziwa au bahari hutegemea uvuvi wa samaki kujipatia kipato na kuendesha maisha yao.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliovutiwa na vipotoshi *A*, *ufugaji wa samaki, B*, *uchimbaji mabwawa* na *D*, *kilimo cha mpunga* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya shughuli za asili zinazofanywa na watu waishio karibu na bahari na maziwa. Pia walishindwa kutofautisha kati ya shughuli za asili na zisizokuwa za asili zinazofanywa na wenyeji waishio karibu na bahari na maziwa. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A*, *Ufugaji wa samaki* na *B*, *Uchimbaji wa mabwawa* walishindwa kutambua kuwa hizo sio shughuli za asili kwani ufugaji wa samaki na uchimbaji wa mabwawa unaweza kufanyika sehemu yoyote bila kujali ukaribu

na bahari au maziwa. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *kilimo cha mpunga* walihusisha maji ya bahari na maziwa na zao la mpunga, kwa kuwa zao hili hulimwa sehemu zenye majimaji, mabondeni na linahitaji maji ili kustawi vizuri japokuwa sio lazima lilimwe karibu na bahari au maziwa. Hata hivyo, maji ya bahari hayafai kwa kilimo cha mpunga kwa sababu yana chumvi nyingi.

(v) Zamani viongozi wa makabila walipatikana kwa njia gani?
- A Kurithishwa
- B Uchaguzi
- C Uteuzi
- D Kupendekeza

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti* na kililenga kubaini namna viongozi wa makabila mbalimbali walivyokuwa wanapatikana. Wanafunzi waliobaini jibu sahihi *A*, *kurithishwa* walikuwa na maarifa ya kutosha na walitambua kuwa makabila mengi yalitumia njia ya kurithisha madaraka ya kuongoza kwa ndugu wa karibu kwenye ukoo husika. Wanafunzi hawa walipata maarifa kuhusu namna viongozi wa zamani wa makabila walivyopatikana kwa njia mbalimbali kama vile kufundishwa, kusoma vitabu vya historia au kuhadithiwa na wakubwa wao.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi, *B, uchaguzi, C, uteuzi na D, kupendekeza*, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu namna viongozi wa makabila mbalimbali walivyopatikana. Aidha, walishindwa kubaini kuwa vipotoshi vyote ni njia za kupatikana kwa viongozi lakini hazikuwa njia sahihi za zamani za kuwapata viongozi wa makabila. Wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha njia mbali mbali za kuwapata viongozi, kwa mfano kipotoshi *B*, *uchaguzi* ni njia ya kupata viongozi kwa njia ya kupiga kura *C, Uteuzi*, ni njia inayotumiwa na mamlaka za uteuzi au mtu aliyepewa jukumu hilo kuteua viongozi kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyobainishwa. *D*, *kupendekeza* ni njia ya kushawishi mamlaka za uteuzi ili kufanya maamuzi kuhusu sifa za mtu kushika nafasi fulani ya uongozi. Njia zote zinaweza


kutumika kupata viongozi kwa nyakati hizi na sio viongozi wa zamani wa makabila walivyopatikana.

### 2.1.2 Kuoanisha maana ya maneno

Swali **la 2:** Jibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha maana ya maneno katika fungu **A** na maneno sahihi katika fungu **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

<table>
<tr><th colspan="2">Fungu A</th><th>Herufi</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>(i)</td><td>Hutoa taarifa kwa njia ya sauti tu.</td><td>(   )</td><td rowspan="4">A. Gazeti<br>B. Maabara<br>C. Maktaba<br>D. Masimulizi<br>E. Redio<br>F. Runinga</td></tr>
<tr><td>(ii)</td><td>Hutoa taarifa kwa njia ya picha na maneno</td><td>(   )</td></tr>
<tr><td>(iii)</td><td>Hutoa taarifa kwa njia ya picha, maneno na sauti.</td><td>(   )</td></tr>
<tr><td>(iv)</td><td>Hutoa taarifa kwa njia ya mazungumzo.</td><td>(   )</td></tr>
</table>

Swali hili lilikuwa na vipengele vinne kutoka katika umahiri mkuu *Kuwa mstahimilivu* na kwenye umahiri mahsusi *Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu*. Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini vyanzo mbalimbali vya taarifa**.** Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo ni asilimia 69.7 ya wanafunzi 1,702,578 ndio waliweza kupata kuanzia alama 4 hadi 8 na asilimia 30.3 ufaulu wao ulikuwa hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2. **Chati Na. 2** inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na.2**: *kiwango kizuri cha ufaulu cha wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele ni kama ifuatavyo:

**Kipengele cha (i)** kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini jina la chombo cha habari kinachotoa taarifa kwa njia ya sauti tu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *E*, *Redio* walikuwa na uelewa juu ya vyombo vya habari ambavyo hutoa taarifa kwa njia ya sauti. Walielewa kuwa redio hutoa taarifa kwa njia ya sauti ambapo ni tofauti na vyanzo vingine kama vile runinga. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Gazeti*, hawakuelewa kuwa gazeti ni chapisho linaloundwa kwa karatasi na hutoa taarifa kwa njia ya picha na maneno pekee. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Maabara,* hawakutambua kuwa maabara ni jengo au chumba ambapo majaribio ya kisayansi na tafiti hufanyika au kufundishia na sio kutoa taarifa kwa sauti. Baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, maktaba* hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kuelewa kuwa maktaba ni jengo linalohifadhi machapisho, vitabu na nyaraka mbalimbali ambapo watu hufika na kujisomea na sio chombo cha kutoa taarifa. Wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi *D, masimulizi* kwa kuwa nayo ni njia mojawapo inayotoa taarifa za matukio halisi au za kubuni zinazohusu hali halisi ya maisha, hivyo walichanganya na utoaji wa taarifa kwa njia ya sauti tu.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi *F, runinga* walishindwa kutambua kuwa *runinga* ni kifaa kinachonasa sauti, maandishi na picha na kuoneshwa kwa watazamaji.

**Kipengele cha (ii)** kiliwataka wanafunzi kutambua vyombo vya habari vinavyoweza kusambaza habari kwa njia ya picha na maneno tu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi A, *Gazeti* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vyombo vya habari vinavyotoa taarifa/habari kwa njia ya maneno na picha. Walielewa vyema kuwa gazeti hutoa taarifa/ habari kwa njia ya maneno na picha. Vilevile, hutoa taarifa zenye maudhui mbalimbali kwa mfano taarifa zinahusu uchumi, kijamii, siasa na Sayansi na teknolojia. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Maabara*, *C, Maktaba*, Hawakuelewa kuwa maeneo hayo ni mahali ambako mtu anafanya utafiti/majaribio ya kisayansi na vilevile machapisho mbalimbali hupatikana hivyo kuongeza maarifa katika maisha mtawalia lakini sio sehemu ya vyombo vinavyotoa taarifa. Wakati vipotoshi D*, Masimulizi*, E*, Redio* na F, *Runinga* ni vyanzo vya taarifa lakini kwa njia tofauti, hivyo walishindwa kutofautisha namna vyombo hivyo vinavyoweza kutoa taarifa/habari. Aidha, waliochagua kipotoshi F, *runinga* walishindwa kutofautisha kwa sababu runinga pia hutoa taarifa kwa njia ya picha, maneno na sauti kwa pamoja lakini swali lililenga picha mnato na sio picha mjongeo.

**Kipengele cha (iii)** kiliwataka wanafunzi kutambua vyombo vinavyotoa taarifa kwa njia ya picha, maneno na sauti. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *F, runinga* walikuwa na uelewa sahihi juu ya vyombo vinavyotoa taarifa kwa njia ya picha, sauti na maneno. Njia hii imeenea sana nchini na familia nyingi zina runinga nyumbani na wanafunzi wengi ni watazamaji wazuri na walikuwa na uwezo wa kuhawilisha maarifa. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Gazeti* hawakuwa na uelewa sahihi wa aina ya chombo kinachotoa taarifa kwa njia ya sauti, maneno na picha. Hawakutambua kuwa gazeti ni chapisho ambalo hutoa taarifa kwa njia ya picha na maneno tu.

Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *B, maabara*, hawakuwa na uelewa unaohusiana na vyombo vinavyotoa taarifa/habari. Maabara ni jengo au chumba kinachohusika na masuala ya tafiti au majaribio ya kisayansi na sio chanzo cha kutoa taarifa au habari.

Kipotoshi *C, maktaba* kilichaguliwa na wanafunzi walioshindwa kuelewa kuwa maktaba ni jengo au chumba maalumu chenye kuhifadhi nyaraka, vitabu na machapisho mbalimbali ambamo watu wanakwenda kusoma au kujisomea na sio chombo kinachotoa taarifa kama yalivyo magazeti, runinga au redio. Wanafunzi hawa walichanganya jengo hili na vyombo vingine vya taarifa/habari kwa sababu ni sehemu ya kujipatia maarifa na ujuzi.


Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *D, masimulizi* hawakuelewa kuwa masimulizi ni njia ya kupata taarifa kwa njia ya mdomo ambayo hutolewa na watu wenye umri mkubwa. Masimulizi hayo yanaweza kuwa ya kweli au sio ya kweli lakini mara nyingi huakisi uhalisia wa maisha ya watu na hayatoi taarifa kwa njia ya picha kama ilivyo runinga. Vilevile, wanafunzi wengine waliochagua *kipotoshi E*, *redio* hawakufahamu kuwa redio haitoi taarifa kwa njia ya picha bali ni chanzo cha taarifa kwa kuwa ni chombo kinachopokea mawimbi sauti na kuyabadilisha kuwa maneno.

**Kipengele (iv)** kiliwataka wanafunzi kubaini njia inayoweza kutumika kufikisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *D, Masimulizi* walikuwa na uelewa sahihi juu ya namna mbalimbali ya kutoa na kupokea taarifa. Walitambua kuwa Masimulizi ni njia ya kutoa taarifa iliyokuwa inatumika miaka mingi iliyopita na ambayo inatumika mpaka miaka ya sasa hivi, ambapo wazee/watu wazima/vijana hukaa na watu wa umri mdogo na kusimulia matukio ambayo yanaweza kuwa ya kweli au la, lakini yenye kuakisi uhalisia wa maisha katika jamii. Masimulizi haya ni aina ya mafundisho yanayotolewa kwa watoto au vijana na kuwa chanzo cha taarifa/habari. Masimulizi yanaweza kuwa ya kutoa tahadhari, kuasa, au kufundisha.

Kwa upande mwingine**,** Wanafunzi waliochagua vipotoshi *A, Gazeti*, *E, redio* na *F, runinga*, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana na umuhimu wa masimulizi kama chanzo cha taarifa/habari kupitia njia ya mazungumzo. Walichanganya kwa kuwa vyote ni vyanzo vya taarifa lakini vyenye kutofatiana kwa namna taarifa/habari zinavyotolewa. Aidha wanafunzi wengine waliochagua vipotoshi *B, maabara* na *C*, *maktaba* wakiamini kwamba vinahusika na kutoa taarifa/habari kama ilivyo kwa masimulizi.

### 2.1.3 Kuchagua jibu sahihi katika mabano

**Swali la 3** Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kuwa Mwadilifu* na vipengele vinne vilitoka katika umahiri mahsusi wa *kuaminika katika jamii* na *kusimamia haki*. Kila kipengele kilikuwa na alama 2. Ufaulu wa wanafunzi katika Swahili hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 991,792 (58,2%) waliweza kupata alama 4 hadi 8. Wanafunzi 319,100 (41.7%) hawakufanya vizuri kwa sababu walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** Kiwango cha Ufaulu cha wanafunzi katika swali la 3 kwa kupata alama 4 hadi 8

Chat Na 3: inaonesha kiwango cha wastani cha ufaulu katika swali la 3 ambapo asilimia 58.3 tu ya wanafunzi waliweza kupata alama kuanzia 4 hadi 8

Kwa upande mwingine uchambuzi unaonesha kuwa, swali la 03 ndilo lililokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu ikilinganishwa na maswali mengine. Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 319,100 sawa na asilimia 41.7 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu katika swali la 3 Kiwango cha ufaulu wa wastani kilikuwa asilimia 58.3. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika vipengele vinne vya maswali ni kama ifuatavyo:

(i) Watoto walitoa ushahidi wa kweli juu ya wizi uliofanywa na wenzao. Kitendo walichofanya watoto kinaonyesha nini?
(uaminifu, upendo, usaliti)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi *kuaminika katika jamii* na kilililenga kupima ufahamu wa mwanafunzi kuhusu dhana na matendo yanayoonesha uaminifu na maadili mema katika jamii na familia. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *uaminifu* walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya uaminifu. Wanafunzi hawa wanaelewa kuwa uaminifu ni hali ya kukubalika au kuaminika kwa watu na unajengwa kwa kutenda matendo kama vile kutimiza ahadi, kusema ukweli, kutunza siri na kufichua uovu ikiwa ni pamoja na hali ya kuishi sawasawa na maadili ya jamii. Aidha, wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi wamefundishwa katika familia zao, shuleni na kusoma machapisho mbalimbali yanayoelezea dhana ya uaminifu na matumizi yake katika jamii.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi walivutiwa na vipotoshi *upendo na usaliti*. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa dhana ya uaminifu katika jamii. Walishindwa kutambua kuwa upendo ni hali ya kuwa na ukaribu kati ya mtu mmoja na mwingine unaoonesha hali ya kujali na kuthamini. Upendo unaweza kuoneshwa kwa kutumia lugha inayofaa, kuwasikiliza wengine na kuwasaidia. Hivyo, kitendo cha watoto kutoa ushahidi wa kweli juu ya wizi uliofanywa na wenzao hakiwezi kutafsiriwa kuwa ni *upendo*. Vilevile, Wanafunzi waliochagua *usaliti* hawakuelewa tafsiri sahihi ya kitendo cha watoto kutoa ushahidi wa ukweli kuhusu wizi uliofanywa na wenzao kwani usaliti ni utoaji wa taarifa za siri za upande mmoja kwa upande mwingine wa maadui.

Hivyo, kwa muktadha wa swali jibu sahihi halikuwa *usaliti* bali ni *uaminifu*.Usaliti katika jamii husababisha matatizo ya ugomvi, kutoaminika, uvunjifu wa amani au kukosa amani. Wanafunzi hawakuwa na ufahamu kuwa uaminifu kinyume chake ni usaliti.

(ii) Mtu ambaye ana umri wa chini ya miaka 18 huitwa
(kijana, mtoto, mtu mzima)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kusimamia haki* na lengo la swali ilikuwa kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini tofauti ya umri wa mtoto na mtu mzima. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *mtoto* waliweza kutofautisha umri wa mtoto na mtu mzima. Wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umri wa mtoto kwamba mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane. Mtu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 katika mazingira ya kawaida anapaswa kuwa chini ya uangalizi wa wazazi na kupata mahitaji muhimu kutoka kwa wazazi. Aidha, mtu chini ya miaka 18 hashirikishwi na jamii katika kutoa maamuzi ya mambo mengi katika jamii mfano, kuchagua viongozi au kuchaguliwa katika nafasi za uongozi katika kijamii.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha walivutiwa na kipotoshi *Kijana* bila kujua kuwa kijana ni mtu wa jinsi ya kike au kiume si mtoto wala si mtu mzima. Wanafunzi walishindwa kutofautisha kwa sababu wakati mwingine katika jamii watu wenye umri kati ya miaka 14 mpaka 45 huitwa vijana hivyo inaonesha kuwa hawakuwa na ufahamu mzuri kuhusu mgawanyo wa umri kuanzia mtoto, kijana na mtu mzima. Waliochagua kipotoshi *mtu mzima* walishindwa kutambua kuwa kisheria mtu mzima ni mtu ambaye ana umri kuanzia miaka 18 na kuendelea na anaweza kupewa majukumu mbalimbali katika jamii kwa mfano kupiga kura na kupewa uongozi katika jamiii. Aidha, mtu ambaye ana umri Zaidi ya miaka 18 anaweza kufanya maamuzi yake binafsi au kuingia mikataba ya kisheria

(iii) Chombo kipi kisicho cha kiserikali kinachohusika na haki za binadamu katika Tanzania?
(TAMWA, Bunge, Polisi)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kusimamia haki* na kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini taasisi zisizo za kiserikali zinazo husika na kulinda na kutetea haki za binadamu nchini Tanzania. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *TAMWA* walikuwa na uelewa wa taasisi zisizo za kiserikali zinazohusika na haki za binadamu nchini.

Taasisi nyingine isiyo ya kiserikali inayohusika na haki za binadamu ni pamoja na kituo cha sheria na haki za binadamu Tanzania (LHRC).

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi *Bunge* na *Polisi.*hawakuweza kutofautisha kati ya kazi za vyombo vya serikali na zile za vyombo visivyo vya serikali vinavyohusika na haki za binadamu. Wanafunzi waliochagua *Bunge* hawakuelewa kuwa bunge ni muhimili wa serikali ambao jukumu lake kubwa ni kutunga sheria, kujadili na kuridhia mikataba na kujadili utekelezaji wa kila wizara. Wanafunzi waliochagua *Polisi* hawakujua kuwa Polisi ni chombo cha dola chenye jukumu la kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

(iv) Mtu kutoaminika kwa wengine yaweza kuwa ni matokeo ya mtu huyo
(kutokuwa muwazi, kuwa mnyenyekevu, kuwa mchapakazi)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *kuaminika katika jamii*, na kililenga kupima uelewa wa wanafunzi juu ya dhana ya uwazi na athari za kutokuwa muwazi. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *Kutokuwa muwazi* walionesha uelewa wa matendo ya kutokuwa muwazi kuwa ni kutosema ukweli au kutotoa taarifa sahihi. Pia waliweza kubaini athari za kutokuwa muwazi kuwa ni kusababisha matatizo makubwa kama migogoro, ugomvi pamoja na uvunjifu wa amani. Aidha, walielewa kuwa uwazi huleta amani, upendo na utuilivu katika jamii. **Kielelezo 3.1** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika majibu sahihi katika swali hili.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Watoto walitoa ushahidi wa kweli juu ya wizi uliofanywa na wenzao. Kitendo walichofanya watoto kinaonyesha nini? Uaminifu
(uaminifu, upendo, usaliti)

(ii) Mtu ambaye ana umri wa chini ya miaka 18 huitwa mtoto
(kijana, mtoto, mtu mzima)

(iii) Chombo kipi kisicho cha kiserikali kinachohusika na haki za binadamu katika Tanzania? TAMWA.
(TAMWA, Bunge, Polisi)

(iv) Mtu kutoaminika kwa wengine yaweza kuwa ni matokeo ya mtu huyo kutokuwa muwazi.
(kutokuwa muwazi, kuwa mnyenyekevu, kuwa mchapakazi)

**Kielelezo 3.1***Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3.*

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *kuwa mnyenyekevu*, hawakujua kuwa unyenyekevu ni tabia chanya aliyonayo mtu kwa Mungu wake au binadamu mwenzake, ikiwa ni pamoja na utiifu, adabu na heshima kinyume na tafsiri ya tabia ya kutoaminika ambayo inaakisi tabia hasi, Waliochagua *kuwa mchapakazi* walishindwa kubaini tafsiri sahihi ya matokeo ya mtu kutoaminika kwa wengine. Mchapakazi ni mtu mwenye kujituma, asiyeshurutishwa, asiyependa kusimamiwa na mwenye moyo wa kufanya kazi kwa bidii. Kwa muktadha huo, jamii inakuwa na mtazamo chanya na mtu mchapa kazi kinyume na mtu asiyeaminika. **Kielelezo 3.2** ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Watoto walitoa ushahidi wa kweli juu ya wizi uliofanywa na wenzao. Kitendo walichofanya watoto kinaonyesha nini? usaliti
(uaminifu, upendo, usaliti)

(ii) Mtu ambaye ana umri wa chini ya miaka 18 huitwa kijana
(kijana, mtoto, mtu mzima)

(iii) Chombo kipi kisicho cha kiserikali kinachohusika na haki za binadamu katika Tanzania? Polisi
(TAMWA, Bunge, Polisi)

**Kielelezo 3.1`**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mwanafunzi katika swali la 3

## 2.2 Sehemu B

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) swali la 4, 5, na 6. Swali la 4 lilikuwa la kuonesha matendo yanayoonesha kujipenda au kuwapenda wengine na lilikuwa na vipengele vinne, kila kipengele kilikuwa na alama 2, jumla ya alama kwa vipengele vyote ni 8. Wanafunzi walitakiwa kuweka alama ya vema (√ ) kwenye sehemu inayohusika. Swali la 5 lilikuwa la kuchunguza picha kisha kujibu maswali yanayofuata. Swali hili lilikuwa na alama 8 na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2, jumla alama 8. Swali la 6 lilikuwa la kusoma kifungu cha habari kisha kujibu vipengele (a) – (d) katika karatasi ya kujibia. Swali hili pia lilikuwa na jumla ya alama 8. Jumla ya alama katika sehemu hii zilikuwa ni 24.


Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 4.

### 2.2.1 Kuoanisha matendo

**Swali la 4:** Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **kujipenda** au **kuwapenda wengine** kwa kuweka alama ya (√) kwenye sehemu inayohusika. Namba (i) imejazwa kama **Kama mfano**.

| Na. | Kitendo | Kujipenda | Kuwapenda wengine |
|---|---|---|---|
| (i) | Subira anawaogesha wadogo zake kila siku. | | √ |
| (ii) | Jumanne anafua sare zake za shule na kuzipiga pasi kila siku. | | |
| (iii) | Juma alimshukuru Roda kwa kutoa msaada kwa mama yake aliyekuwa mgonjwa. | | |
| (iv) | Amina anapiga mswaki na kuoga kila siku. | | |
| (v) | Mwanafunzi alitoa pole kwa mwenzie aliyepata matatizo. | | |

Swali lilikuwa na vipengele vinne; (ii) (iii), (iv) na (v), vilivyotoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu jamii,* kwenye umahiri mahsusi *kujipenda na kuwapenda watu wengine*. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kutambua matendo ya kujipenda au kuwapenda watu wengine. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 1,244,064 (73.1%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8, na wanafunzi 458,514 (26.9%) walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2. **Chati Na. 4** inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4:** *kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali la 4 kwa kupata alama kati ya 4 hadi 8.*

**Kipengele** (ii) kiliwataka wanafunzi kubaini kama kitendo cha *Jumanne kufua sare zake za shule na kuzipiga pasi kila siku* ni kitendo cha kujipenda au kuwapenda wengine. Wanafunzi waliobainisha kuwa kitendo hicho ni cha kujipenda, walikuwa na maarifa ya kutosha kuweza kutofautisha dhana ya kujipenda na kuwapenda wengine. Walielewa kuwa kujipenda ni kujithamini na kujikubali na waliamini kwamba mtoto anayejipenda anatunza afya yake na anaepuka matendo mabaya na anakuwa na tabia njema wakati wote.

Aidha, wanafunzi walioshindwa kubaini kuwa kufua sare za shule na kuzipiga pasi kila siku kunaonesha kujipenda, hawakujua kuwa kujipenda ni tendo la hiari ambalo mtoto anatenda katika maisha yake ya kila siku mfano kupiga mswaki, kuvaa nguo safi, kupiga pasi na kufua nguo zake. Pia walishindwa kutofautisha kati ya dhana ya kujipenda na kuwapenda watu wengine.

**Kipengele** (iii) kiliwataka wanafunzi kuonesha kama kitendo cha *Juma kumshukuru Roda kwa kutoa msaada kwa mama yake aliyekuwa mgonjwa*, ni kitendo cha kujipenda au kuwapenda wengine. Wanafunzi waliochagua kuwapenda wengine walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya kujipenda na kuwapenda

wengine. Walielewa kuwa kuwapenda watu wengine huhusisha nafsi ya pili au ya tatu, mfano kuwasalimia wengine kwa lugha inayofaa, kuwasilikiza na kuwaonesha upendo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua *Juma alimshukuru Roda kwa kutoa msaada kwa mama yake aliyekuwa mgonjwa* kama kitendo cha kujipenda, walishindwa kutofautisha kati ya kujipenda na kuwapenda wengine. Wanafunzi hao walishindwa kutambua kuwa dhana ya upendo inagawanyika hasa pale wanapofanya matendo mbalimbali ya kujipenda na kuwapenda wengine. Hawakuelewa kuwa mwanafunzi anayependa wengine anakuwa tayari kuwasiliana nao na kuwasaidia, hivyo kuishi vizuri na wengine katika jamii. Kuwapenda wengine hakuhusishi matendo ya nafsi ya kwanza, bali nafsi ya pili au ya tatu.

**Kipengele** (iv) Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu dhana ya kujipenda na kuwapenda wengine waliweza kubaini kuwa *Amina anapopiga mswaki na kuoga kila siku* ni kitendo cha kujipenda. Walikuwa na uelewa kuwa kujipenda huhusisha nafsi ya mtu mmoja. Hujionesha kwa kutenda matendo binafsi yanayo husisha nafsi yako kwa mfano kuoga, kupiga pasi nguo, na kuvaa nguo zenye staha.

Kwa upande mwingine, Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi, kwa kuchukulia kitendo cha Amina *kupiga mswaki na kuoga kila siku* kama kitendo cha kuwapenda wengine, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana ya kujipenda na kuwapenda wengine. Hawakufahamu kuwa kujipenda ni kuvutiwa na kitu, jambo au mtu kutokana na ubora au uzuri wake. Hujionesha kwa kutenda matendo binafsi yasiyo husisha upande wa pili au nafsi ya pili. Amina kupiga mswaki na kuoga kila siku kunahusisha nafsi ya kwanza na wala sio nafsi ya pili au ya tatu.


**Kipengele** (v) Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu dhana ya kujipenda na kuwapenda wengine waliweza kubaini kuwa *Mwanafunzi anapotoa pole kwa mwenzie aliyepata matatizo* ni kitendo cha kuwapenda wengine*. Wanafunzi* hawa walielewa kuwa kuwapenda wengine au wenzao wanapopatwa matatizo inahusisha nafsi ya pili au ya tatu. Wanaopatwa na matatizo hujaliwa kwa kuwa ni njia mojawapo ya kuwatia moyo au

kuwafariji. Pia walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa unapotoa msaada ni ishara ya kuwapenda wengine na ni jambo la kheri. Vilevile, wanafahamu kuwa kuwapenda wengine ni jambo linalosisitizwa ili kuishi vizuri na wanajamii. Mifano ya matendo ya kuwapenda wengine ni kama vile kumnyamazisha mdogo wako anapolia, kumsaidia mtu asiyeona na kumwazima kalamu mwenzako darasani ambaye hana.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua *Mwanafunzi alitoa pole kwa mwenzie aliyepata matatizo,* kama kitendo cha kujipenda walionesha kukosa uelewa wa kutosha wa tofauti ya kujipenda na kuwapenda wengine. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa mtu anapotoa pole kwa mwenzie aliyepata matatizo, kumsalimia mwalimu anapoingia darasani na mwanafunzi anaposalimia wakubwa wake au kumsaidia mwanafunzi mwenzake aliyeanguka hudhihirisha kuwa na matendo yanayoonesha kuwapenda wengine na sio kujipenda kama wanafunzi wengine walivyoonesha.

### 2.2.2 Kuchunguza picha

**Swali la 5:** Swali hili liliwataka wanafunzi kuchunguza kwa makini picha na kisha kujibu maswali yanayofuata.



**Maswali**

(a) Ni rasilimali gani inaharibiwa katika picha hii?

______________________

(b) Ni njia gani wanatumia kuharibu rasilimali iliopo kwenye picha hii?

_______________________________


(c) Ni kifaa gani wanatumia kuharibu rasilimali hii?

_________________________

(d) Uharibifu wa rasilimali hii husababisha nini?

_______________________________

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira.* Swali lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu madhara yatokanayo na ukataji miti ovyo. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi 1,161,104 (68.2%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8, na wanafunzi 541,474 (31.8%) walipata alama kuanzia 0 hadi 2 kama inavyooneshwa kwenye chati.Na.5




**Chati Na.5:** *Kiwango kizuri cha ufaulu cha wanafunzi katika swali la 5*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(a) Ni rasilimali gani inaharibiwa katika picha hii? ____________________

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu aina ya rasilimali inayoharibiwa. Wanafunzi waliojibu *Miti* walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya rasilimali inayoharibiwa. Miti ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya kila siku ya binadamu na viumbe vingine vilivyo hai. Aidha, miti husaidia kuzuia tatizo la mmomonyoko wa udongo na ukame.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao walipata alama 0 katika kipengele hiki, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo kutoa aina mbalimbali za majibu ambayo siyo sahihi kama vile*, uharibifu wa mazingira, kukata miti au mimea, mkaa, mmomonyoko wa udongo na anabumzkia.* Wanafunzi waliotaja *Uharibifu wa mazingira w*alishindwa kubaini rasilimali iliyokuwa inaharibiwa hivyo kutoa majibu ya jumla. Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, wanyama, wadudu, maji na mimea. Wanafunzi wengine walitaja *kukata miti w*alishindwa kutofautisha aina ya rasilimali iliyokuwa inaharibiwa na njia inayotumika kuharibu rasilimali. Vilevile, wanafunzi *waliyotaja mkaa w*alikosa ufahamu kuwa *Mkaa* ni bidhaa inayotengenezwa baada ya miti kukatwa. Wanafunzi walioandika *mmomonyoko wa udongo* pia walishindwa kutofautisha matokeo ya uharibifu wa rasilimali ambayo ni mmomonyoko wa udongo na kubaini aina ya rasilimali iliyokuwa inaharibiwa katika picha. Aidha, wengine walikosa stadi za KKK hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka.mfano *anabumzkia.*

(b) Ni njia gani wanatumia kuharibu rasilimali iliopo kwenye picha hii?______________________________

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu njia inayotumika kuharibu rasilimali iliyopo katika picha. Wanafunzi wenye ufahamu wa kutosha waliweza kubaini njia inayotumika kuharibu rasilimali hiyo kuwa ni *kukata miti.*

Njia hii hutumika ili kutimiza malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata mahitaji ya nishati ya mkaa, kupata mbao kwa ajili ya ujenzi na kuandaa mashamba mapya.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 0 walishindwa kubaini matakwa ya swali kwa kuandika aina mbalimbali za majibu kama vile; *shoka, wachome moto, kushirikiana, kutengeneza mkaa na vifaa*. Wanafunzi wengine waliandika *shoka* walishindwa kutofautisha kifaa kinachotumika kukata miti na matakwa ya swali yaliyowataka kutaja njia inayotumika kuharibu rasilimali, wanafunzi waliotaja njia ya *kuchoma moto* walishindwa kubaini vitendo vinavyofanyika katika picha na hivyo kutumia uzoefu wao binafsi. Vilevile, wanafunzi walioandika *kushirikiana* walishindwa kutafsiri sawasawa vitendo vya watu watatu kwenye picha waliyopewa. Aidha, wanafunzi walioandika *kutengeneza mkaa* walishindwa kubaini matakwa ya swali. Swali liliwataka kubaini njia ambayo ilitumika katika picha kuharibu rasilimali badala ya kueleza matumizi ya miti. Mwisho, wanafunzi walioandika *vifaa* vilevile walishindwa kuelewa matakwa ya swali.

(c) Ni kifaa gani wanatumia kuharibu rasilimali hii?

____________________________

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu kifaa kinachotumika kuharibu rasilimali katika picha waliyopewa. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha waliweza kubaini kifaa hicho kuwa ni *shoka.* Wanafunzi hawa walijua shoka ni kifaa kinachotumika kukata miti. Waliona kifaa hicho na kukitambua kwa jina kama shoka.


Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 0 katika kipengele hiki baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine kushindwa kutaja jina la kifaa kilichotumika kuharibu rasilimali kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitaja kifaa hicho kama *utupaji taka ovyo*, mwingine alitaja kifaa hicho kuwa ni *jembe.* Vilevile, wanafunzi wengine walitaja *chenso.* Wanafunzi waliotaja *utupaji taka ovyo w*alishindwa kutumia picha waliyopewa kubaini matakwa ya swali hivyo kutoa jibu ambalo halikuwa sahihi. Vilevile, wanafunzi waliotaja *jembe w*alishindwa kutumia picha waliyopewa

kubaini kifaa kilichotumika kuharibu rasilimali. Jembe hutumika kulimia na siyo kukata miti. Mwisho, badhi ya wanafunzi walitumia uzoefu wao na kutaja *chenso.* Chenso ni neno la kiingereza lililotoholewa likimaanisha *chainsaw*. Hii ni mashine maalum ya kisasa inayotumika kukata miti. Kwa bahati mbaya picha aliyopewa ilikuwa haina picha ya mashine hiyo.

(d) Uharibifu wa rasilimali hii husababisha nini?

____________________________

Kipengele hiki kilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu madhara ya uharibifu wa rasilimali iliyooneshwa katika picha. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha waliweza kubaini matokeo ya uharibifu wa rasilimali kuwa ni *ukame, jangwa, kutokupatikana mvua kwa wingi.* Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa kuhusu faida za utunzaji wa mazingira na rasilimali zake. Vile vile waliweza kutaja madhara yanayoweza kutokea endapo jamii haitachukua tahadhari za kutunza mazingira. **Kielelezo Na.5.1** kinaonesha majibu sahihi ya mwanafunzi.



**Maswali**

(a) Ni rasilimali gani inaharibiwa katika picha hii? miti

(b) Ni njia gani wanatumia kuharibu rasilimali iliopo kwenye picha hii?

kukata miti


(c) Ni kifaa gani wanatumia kuharibu rasilimali hii? shoka

(d) Uharibifu wa rasilimali hii husababisha nini? ukame

**Kielelezo Na.5.1** Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 5.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 0 walishindwa kubaini athari za uharibifu wa rasilimali kwa kutoa majibu kama vile *ulimaji, kukata miti ovyo, kuota mimea, kuchoma misitu na kukosa hewa.* Wanafunzi waliotaja kwa mfano *ulimaji w*alitumia uzoefu wao kuwa wakulima wanapoandaa shamba jipya huanza na ukataji miti. Vilevile wanafunzi waliotaja *kukata miti ovyo, kuchoma misitu na kukosa hewa* walishindwa kubaini matakwa ya swali. Majibu haya yanaashiria kuwa wanafunzi hawakuwa na maarifa ya kutosha

kuhusu elimu ya utunzaji mazingira. **Kielelezo Na. 5.2** kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili.



Maswali

a) Ni rasilimali gani inaharibiwa katika picha hii? ifuatayo

b) Ni njia gani wanatumia kuharibu rasilimali iliopo kwenye picha hii?

rasilimali

c) Ni kifaa gani wanatumia kuharibu rasilimali hii? ya wezo

d) Uharibifu wa rasilimali hii husababisha nini? matokeo

**Kielelezo Na. 5.2:** *sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5.*

### 2.2.3 Kusoma kifungu cha habari

Swali **la 6:** Swali hili liliwataka wanafunzi kusoma kwa makini kifungu cha habari kisha kujibu maswali.


*Shule ni mahali ambapo ufundishaji na ujifunzaji hufanyika. Matendo ya ufundishaji na ujifunzaji ni kama vile kuhesabu, kusoma, kuandika, kuchora, kucheza na kuonesha tabia njema.*

*Tunakwenda shuleni mapema asubuhi na kufanya usafi kwenye mazingira ya shule. Kengele ikigongwa, tunasimama kwenye mistari na kusikiliza matangazo mbalimbali. Baada ya hapo tunaingia madarasani tayari kuanza masomo saa mbili kamili asubuhi.*

*Kila Ijumaa ni siku ya michezo. Tunamaliza masomo saa 6 kamili. Tunakwenda viwanjani kushiriki katika michezo. Tunacheza michezo ya aina tofauti kama vile mpira wa miguu, mpira wa mikono, kuteleza, ukuti, kukimbia na kubembea*.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwa mstahimilivu* na umahiri mahsusi wa *kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu*. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Swali lililenga kubaini uwezo wa wanafunzi wa kutafuta taarifa kutoka vyanzo tofauti. Vilevile swali lililenga kubaini shughuli zinazofanyika shuleni na namna ya kupata taarifa sahihi. Ufaulu wa

wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo asilimia 67.8 ya wanafunzi 1,702,578 walikuwa na alama kuanzia 4 hadi 8. Asilimia 32.2 ya wanafunzi walikuwa na alama kuanzia 0 hadi 2. Kwa ujumla, kiwango hiki cha ufaulu ni cha kati ya wastani hadi kizuri sana kama inavyoonekana katika **chati 6**




**Chati Na.6**: *Kiwango cha wastani cha ufaulu cha wanafunzi katika swali la 6*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(a) Taja shughuli kuu mbili zinazofanyika shuleni.

(i) ______________________

(ii) ______________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja shughuli kuu mbili zinazofanyika shuleni na kalilenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu shughuli muhimu zinazofanyika shuleni. Wanafunzi walioweza kukielewa vema kifungu cha habari waliandika majibu sahihi kuwa ni *ujifunzaji na ufundishaji.* Wanafunzi hao walitambua kuwa shughuli kuu inayo wapeleka shuleni ni ujifunzaji ambao unafanikishwa na walimu wanaowafundisha. Pia, Wanafunzi waliweza kubaini kuwa ili ujifunzaji ufanikiwe lazima kuwepo na ufundishaji kama ilivyo katika shule zote kwamba kuna walimu wanaofundisha na wanafunzi wanaojifunza.

Hivyo kuwa kimsingi kunakuwepo shughuli kuu mbili shuleni ambazo hujumuisha walimu kwa upande mmoja na wanafunzi kwa

upande mwingine. Aidha, wanafunzi waliotoa majibu sahihi kwa kipengele hiki wana uwezo mzuri wa kusoma kifungu cha habari na kufahamu ujumbe uliomo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kuelewa kifungu cha habari walitoa majibu ambayo si sahihi kama vile; *kuteleza, mpira wa mikono, kufanyakazi kwenye mazingira*, *kusoma kwa bidii, kukata miti* n.k. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa uelewa wa kusoma na kubaini maudhui yaliyopo kwenye kifungu cha habari.

(b) Ni kwanini wanafunzi husimama kwenye mistari kila kengele inapogongwa? ____________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja sababu ya wanafunzi kusimama kwenye mistari kila kengele inapogongwa. Wanafunzi waliosoma na kuelewa kifungu cha habari waliweza kuandika jibu sahihi *kusikiliza matangazo mbalimbali*. Walielewa kuwa kengele ni kiashiria cha kutaka kutoa taarifa kwa wanafunzi ndio maana hukusanyika.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi hawakuelewa kifungu cha habari na waliandika majibu mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi kama vile; *kukimbia na kubembea*, *ujifunzaji hufanyika matendo ya ufundishaji, ukuti* n.k. Wanafunzi hawa wanaonesha kuwa walikuwa hawashiriki katika baadhi ya shughuli za darasani kama vile kusoma vifungu vya habari na kuibua maudhui yaliyomo.


(c) Ni muda gani vipindi huanza? ______________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja muda wa kuanza kwa vipindi. Lengo la swali hili lilikuwa kuwataka wanafunzi kubaini muda au ratiba ya shule kwa juma zima na kwa kila siku ikihusisha muda wa kuanza vipindi vya darasani. Wanafunzi waliosoma kwa makini kifungu cha habari walibaini jibu sahihi kuwa *vipindi huanza saa 2 kamili*. Vilevile, wanafunzi hao walidhihirisha kuwa walikuwa wanashiriki kufanya mazoezi ya kusoma vifungu vya habari kisha kuibua maudhui yake wakiwa shuleni.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache hawakuelewa wala hawakuwa na maarifa ya kufahamu maudhui kutoka kwenye kifungu cha habari na hivyo kuandika majibu mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi kama vile *tunacheza michezo mbalimbali*, *mpira wa miguu, kubembea, tunamaliza*, *saa moja*, *masomo* nk. Aidha, wanafunzi wengine waliacha nafasi bila kuandika chochote.

(d) Ni siku gani masomo huisha saa 6 kamili? ______________________


Lengo la kipengele lilikuwa kuwataka wanafunzi wabaini ratiba nzima ya siku, kwa kuwa ratiba ya juma haifanani kwa siku zote za juma. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu mzuri waliweza kutambua jibu sahihi kuwa ni siku ya *Ijumaa*. Walielewa siku hiyo baada ya saa 6 wanafunzi hushiriki katika michezo mbalimbali viwanjani. Wanafunzi walioandika jibu sahihi walionyesha umahiri wa kusoma kwa ufahamu ambapo mwanafunzi wanasoma matini na kuelewa ujumbe uliokusudiwa. **Kielelezo Na.6** ni sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 6


Maswali
(a) Taja shughuli kuu mbili zinazofanyika shuleni.
(i) Kujifunza
(ii) Ufundishaji
(b) Ni kwanini wanafunzi husimama kwenye mistari kila kengele inapogongwa?
Kusikiliza maelekezo
(c) Ni muda gani vipindi huanza? Saa mbili kamili
(d) Ni siku gani masomo huisha saa 6 kamili? Ijumaa

**Kielelezo Na 6:** *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 6*

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache hawakuelewa kifungu cha habari kwa kuandika majibu kama vile, *mpira, siku ya januari, ijumaa saa 6:30, hadi saa nane* n.k. Lakini pia walishindwa kuhawilisha mazoea ya kila siku shuleni kwamba wanatoka mapema siku ya Ijumaa. Na hii inaonyesha pia uwezo wao katika kipengele cha kusoma kwa ufahamu kuwa ni mdogo. Kati yao wengine hawakuwa na stadi za KKK na hivyo kushindwa kusoma na kuandika majibu yanayoelewaka.

**Kielelezo Na. 6.1.** Kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi katika swali hili.


**Maswali**

(a) Taja shughuli kuu mbili zinazofanyika shuleni.

(i) kufanyausafi

(ii) kunyeshele amaua ayashule

(b) Ni kwanini wanafunzi husimama kwenye mistari kila kengele inapogongwa?

wimbawataifa

(c) Ni muda gani vipindi huanza? saa: 2: 30 hahusu

(d) Ni siku gani masomo huisha saa 6 kamili? ijumaa saa 6:30

**Kielelezo Na. 6.1***: sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa kati ya aina 5 za umahiri zilizopimwa aina 4 za umahiri zimekuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Umahiri huo ni *kudumisha amani* katika swali la 1 (73.6%), *Kuheshimu Jamii* katika swali la 4 (73.1%), *Kuwa Mstahimilivu* katika swali la 2 na 6 (68.8%), *Kuithamini Jamii* katika swali la 5 (68.2%). Kwa upande mwingine, umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* katika swali la 3 umekuwa na ufaulu wa wastani (58.3%).

Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kati ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2019 na 2020 unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kudumisha Amani* kimeongezeka kutoka ufaulu wa wastani (59.8%) mwaka 2019 na kufikia kiwango cha ufaulu mzuri (73.6%) mwaka 2020. Kiwango cha ufaulu katika umahiri mwingine kiliongezeka kama ifuatavyo; *Kuithamini Jamii* uliongezeka kutoka kiwango cha wastani (61.9%) na kuwa kiwango

kizuri (68.2%). Aidha, ufaulu katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* Ulishuka ubora wake kutoka kiwango kizuri (79.6%) mwaka 2019 na kuwa kiwango kizuri cha ukingoni (68.8%) mwaka 2020. Vilevile, kiwango cha ufaulu katika Umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* kiliendelea kuwa cha wastani (59.7%), (58.3%) kwa miaka yote miwili mfululizo 2019 na 2020 mtawalia. Mwisho, umahiri wa *Kuiheshimu Jamii* ingawa haukupimwa mwaka 2019 ulikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu (73.1%) kwa mwaka 2020. Taarifa zaidi za ufaulu wa wanafunzi zimeambatanishwa katika *Kiambatisho A.*

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili umeonesha kuwa, kwa ujumla, wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri cha asilimia 95.46. Wanafunzi waliofanya vizuri katika upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa. Aidha, waliweza kubaini matakwa ya maswali mbalimbali yaliyoulizwa na pia walimudu vyema stadi za Kusoma na Kuandika

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi, Baraza la Mitihani linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu waongeze juhudi kwa kutumia mbinu mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji wa umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* ambao umekuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Mbinu hizo ni pamoja na :

(i) Matumizi ya igizo dhima ili kuwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu kutambua matendo ya kukosa uaminifu.

(ii) Kutumia mbinu ya ufundishaji na ujifunzanji kwa njia ya hadithi fupi kuonesha manufaa ya kuwa mkweli na muwazi.

(iii) Kutumia chati mbalimbali wakati wa kufundisha na kujifunza kuonesha tofauti ya matendo yanayojenga tabia ya kuwa na uaminifu na kukosa uaminifu.

(iv) Kutumia vielelezo vya picha katika kuonesha matendo mbalimbali wakati wa kujifunza.

(v) Kutumia wageni/wataalamu waalikwa katika kutoa ufafanuzi wa umahiri wa aina mbalimbali.

(b) Walimu waandae mazoezi, majaribio na mitihani mara kwa mara ambayo hukuza uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayopima stadi mbalimbali kama vile Kuandika, Kusoma, Kufikiri na Ubunifu.

(c) Wanafunzi wahamasishwe na kuongozwa katika kusoma vitabu vya kiada na rejea ili kuongeza uelewa wao katika umahiri mbalimbali wa somo hili.

(d) Katika ufundishaji na ujifunzaji wa Umahiri wa *Kuwa mwadilifu*, Walimu waweke msingi wa uwezo wa kudadisi, kufikiri, kusikiliza, kuuliza maswali, kuchambua na kuwasiliana kwa kujiamini kufanya uchunguzi, kufanya majadiliano na uwezo wa kufafanua hoja.

*Kiambatanisho A*

**Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2019 na 2020**

| | **Umahiri** | **UPIMAJI 2019** | | | | **UPIMAJI 2020** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** |
| | | **Namba ya swali** | **% wa ufaulu** | | | **Namba ya swali** | **% wa ufaulu** | | |
| 1 | Kuwa Mstahimilivu | 1 | 79.6 | 79.6 | Vizuri | 2<br>6 | 69.7<br>67.8 | 68.8 | Vizuri |
| 2 | Kuithamini Jamii | 5<br>6 | 57.5<br>66.3 | 61.9 | Wastani | 5 | 68.2 | 68.2 | Vizuri |
| 3 | Kudumisha Amani | 4 | 59.8 | 59.8 | Wastani | 1 | 73.6 | 73.6 | Vizuri |
| 4 | Kuwa Mwadilifu | 3 | 59.7 | 59.7 | Wastani | 3 | 58.3 | 58.3 | Wastani |
| 5 | Kuwa Mwajibikaji | 2 | 44 | 44 | Wastani | | | | |
| 6 | Kuheshimu Jamii | | | | | 4 | 73.1 | 73.1 | Vizuri |